

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com



## MATANGAZO: DOMINIKA 32 YA MWAKA - 09.11.2025

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA 09.11.2025 | **DOMINIKA YA 32 YA MWAKA C**<br>**MAVUNO KILELE PAROKIA & DOMINIKA YA ZAKA**<br>Mchango wa pili kwa ajili ya ujenzi |
| 2. | JUMATANO 12.11.2025 | Kumbukumbu ya Mt. Yosafati wa Polotski, Askofu na Mfiadini |
| 3. | IJUMAA 14.11.2025 | Utafanyika uchaguzi wa Kamati Tendaji za Kwaya zote Saa 10:00 jioni - Kwaya ya Mt. Yohane Paulo II, Kwaya ya Vijana, Kwaya ya Mt. Kizito na Kwaya ya Mt. Antoni wa Padua. |
| 4. | JUMAMOSI 15.11.2025 | Kutakuwa na Misa ya kuhitimisha matembezi ya Sanamu ya Bikira Maria katika **Kanda H** saa 1:00 asubuhi katika **Jumuiya ya Timotheo nyumbani kwa Theofil Mfala** na kukabidhi Sanamu kwa **Kanda I**. Jumuiya zihimize na kufuatilia bahasha za Kapu la Mama na kuzirejesha katika Misa za kuhitimisha matembezi ya sanamu. |
| 5. | JUMAMOSI 15.11.2025 | Utafanyika uchaguzi wa Kamati Tendaji ya Kanda B (Uchaguzi umelazimika kurudiwa kutokana na dosari kwenye uchaguzi uliofanyika. Wanakanda wapange sehemu ya kukutana na kutoa taarifa kwa kamati Tendaji<br>Ukwakata Parokia na Watumishi wa Altare saa 10:00 jioni. Wahusika kwa upande wa Ukwakata ni viongozi wa kwaya zote na kwa upande wa atumishi ni watumishi wote. |
| 6. | JUMAPILI 16.11.2025 | Utafanyika uchaguzi wa Kamati Tendaji wa Vyama wa Kitume ngazi ya Parokia vya Uwaka na Wawata mara baada ya Misa ya Kwanza. Wahusika ni viongozi wote wa Kamati Tendaji wa Uwaka na Wawata ngazi ya Jumuiya. |
| 7. | DOMINIKA 16.11.2025 | **DOMINIKA YA 33 YA MWAKA C**<br>**Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Jumuiya ya Mt. Filipo Mtume<br>Watangaza Neno: Pius Lasway na Sabas Shayo<br>**Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Jumuiya ya Mt. Martha<br>Watangaza Neno: Magreth Bundala na Bertha Maiko<br>**Michango yote ni kwa ajili ya Caritas**<br>**Misa ya 3:** Misa ya watoto Wasimamiazi ni Jumuiya ya Mt. Filipo na |

CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| | | Martha.<br>**Michango yote ni kwa ajii ya Caritas** |
| 8. | UCHAGUZI WA UTOTO MTAKATIFU | Kila Jumuiya inatakiwa kuchagua na kuwasilisha majina ya walezi wawili wa Utoto Mtakatifu (mwanamume na mwanamke) leo ofisini 09.11.2025, na uchaguzi wa viongozi wa Utoto Mtakatifu ufanyike kwa Jumuiya zote mwisho 15.11.2025. Kwa upande wa Viongozi wa Utoto wanakuwa 6 ikiwepo nafasi ya Mtunza hazina Msaidizi. |
| 9. | BAHASHA ZA MFUKO WA UINJILISHAJI - PAPA | Tumepokea bahasha za Marafiki wa Mashirika ya Uinjilishaji ya Baba Mtakatifu (PMS), kila Jumuiya iligawiwa kati ya Bahasa 2 au 3 Dominika iliyopita. Ambao bado hawajachukua wanaombwa kuchukua leo. Mwisho wa kurejesha ni tarehe 30.11.2025. |
| 10. | KUWAOMBEA MAREHEMU | Mwezi Novemba ni mwezi wa kuwakumbuka na kuwaombea marehemu wetu. Fomu za kuwaombea zimetolewa na tutatakiwa kuweka sadaka ya nia ya kuwaombea katika Misa. Fomu na sadaka ziwekwe kwenye bahasha na kufungwa.<br><br>Jumamosi ya 15.11.2025, tutafanya usafi katika makaburi ya Kibaoni mara baada ya sala za Jumuiya, saa 2:00 asubuhi. Kanda na Jumuiya zihamasishe waamini kushiriki kwa wingi. |
| 11. | MAREJESHO YA VITABU | Jumuiya zinakumbushwa kufanya malipo ya vitabu vya Liturujia ya Sikukuu ya sikukuu ya Parokia tarehe 10.08.2025. |
| 12. | UGENI WA KWAYA | Dominika ijayo tarehe 16.11.2025 tutakuwa na ugeni wa Kwaya ya Mt. Gregory Mkuu kutoka Parokia ya Chamazi - Dekania ya Mbagala. Watakuja hapa Parokiani kwetu kuinjilisha na wataimba katika Misa ya 1 & 2. Wenyeji wao ni Kwaya ya Mt. Kizito. |
| 13. | MAADHIMISHO YA MISA YA WAFU KATIKA JIMBO KUU LA DSM SIKU YA JUMATATU TAREHE 10.11.2025 | Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la DSM, Mhashamu sana Jude Thaddeus Ruwa'ichi OFMCap, anawaalika Mapadri, Watawa na Waamini Walei wa Jimbo Kuu la DSM kuadhimisha Misa ya Wafu kwa nia ya kuwaombea pumziko la milele ndugu zetu marehemu waliouawa wakati wa uchaguzi mkuu wa Tanzania uliofanyika tarehe 29.10.2025;aidha katika Misa hiyo pia iwepo nia ya kuwaombea uponaji wote waliojeruhiwa katika tukio hilo.<br><br>Hivyo, Misa zote za siku ya Jumatatu tarehe 10.11.2025 katika Prokia zote na vituo vyote vya Kanisa katika Jimbo Kuu la DSM ziwe kwa ajili ya nia hiyo. |
| 14. | WARSHA YA WAAMINI WOTE JIMBO | Warsha ya waamini wote wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam itafanyika Jumamosi 29.11.2025 katika viwanja vya Parokia ya Kristo Mfalme Tabata kuanzia saa 2:00 asubuhi. Kutakuwa na Mada mbili,<br>1. Uchaguzi/Uongozi katika Kanisa 2. Mwaka wa Jubilei Kuu<br>Kutakuwa pia na vyeti kwa wenye Jubilei za miaka 25, 50 na 75.<br>**Sasa ada ya ushiriki imeondolewa, ushiriki ni bure, tujiandikishe** |

CS CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| | | **kwa wingi. Watakaoshiriki watachangia nauli sh. 5,000/=.** ***Kila Jumuiya inatakiwa kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya uandikishaji washiriki wa Warsha kwani inatakiwa Jimboni.*** |
| 15. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini Letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

***Kauli Mbiu ya Mwaka wa Jubilei Kuu: "Jubilei 2025 – Mahujaji wa Matumaini."***

**MATEMBEZI YA SANAMU YA BIKIRA MARIA KATIKA MWEZI WA ROZARI NA KAMPENI YA KAPU LA MAMA MARIA 2025**

| WIKI | TAREHE | KANDA HUSIKA | MSA YA HITIMISHO |
|---|---|---|---|
| 1 | 28/09 - 04/10 | A | SAA 1:00 ASUB |
| 2 | 04/10 – 11/10 | B | SAA 1:00 ASUB |
| 3 | 11/10 – 18/10 | C | SAA 1:00 ASUB |
| 4 | 18/10 – 25/10 | D & E | SAA 1:00 ASUB |
| 5 | 25/10 – 01/11 | F & G | SAA 1:00 ASUB |
| 6 | 01/11 – 08/11 | H | SAA 1:00 ASUB |
| 7 | 08/11 – 15/11 | I | SAA 1:00 ASUB |
| 8 | 15/11 – 22/11 | J | SAA 10:00 JIONI |
| 9 | 22/11 – 29/11 | K | SAA 10:00 JIONI |

**TANGAZO LA DARAJA YA UPADRE KWA MARA YA KWANZA**

Mhashamu Sana Askofu Mkuu Jude Thaddeus Ruwa'ichi OFMCap wa Jimbo Kuu la DSM anatangaza **Daraja ya Upadri** wa Shemasi **Nicholaus Paschal Nkoronko**, **SDS** wa Shirika la Mungu Mwokozi - Wasalvatoriani kutoka Parokia ya Kigamboni katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam, anayetarajiwa kupewa Daraja Takatifu ya Upadri tarehe 29.11.2025 katika Kanisa la Mt. Yakobo Mtume, Nyumba ya Masista Wasalvatoriani - Migongo, Jimbo la Tunduru Masasi.

**MASOMO DOMINIKA – DOMINIKA YA 33 YA MWAKA C - 16.11.2025**

| | |
|---|---|
| SOMO I | 2 Sam.5:1-3 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 122:1-5 |
| SOMO II | Kol.1:11-20 |
| SHANGILIO | Mk. 1:10 |
| INJILI | Lk 23:35-43 |

CS CamScanner